

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MKOA WA DAR ES SALAAM**

Anwani ya Simu:  
Simu: 2203156/58  
Fax: +25522203213  
Tovuti: [www.dsm.go.tz](http://www.dsm.go.tz)  
Barua Pepe: [ras@dsm.go.tz](mailto:ras@dsm.go.tz)



**OFISI YA MKUU WA MKOA**  
**3 Barabara ya Rashidi**  
**Kawawa,**  
S.L.P 5429,  
**12880 -DAR ES SALAAM.**  
**Tanzania**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

**RC MAKONDA AJITOLEA KUMSAIDIA KIJANA MWENYE TATIZO  
LA UTI WA MGONGO**

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhe. PAUL MAKONDA amejitolea kumsaidia Kijana AHMED ALBAITY anayesumbuliwa na tatizo la Uti wa Mgongo lililompelekea kulala kitandani kwa takribani miaka 10.

AHMED ALBAITY anatakiwa kwenda kutibiwa Nchini China kwa muda wa Wiki tatu akiambatana na Wasaidizi Wawili ambapo Gharama za Matibabu zinazohitajika ni zaidi ya Dola 40,000 za Marekani ambapo Sindano moja aliyoandikiwa inagharimu kiasi cha Dolla 27,000.

RC MAKONDA amesema atafanya jitihada zote kuhakikisha AHMED anapatiwa Matibabu ili aweze kupona na kutimiza ndoto zake akiwa na Afya Njema.

Mapema leo RC MAKONDA ametembelewa Ofisini kwake na Balozi Mpya wa China Nchini Tanzania Bi. WANG KE ambae amekuja kujitambulisha kwa Mkuu wa Mkoa ambapo katika Mazungumzo RC MAKONDA amemgusia Balozi huyo Suala la Matibabu ya AHMED ALBAITY ambapo Balozi WANG KE alieambatana pia na Daktari Bingwa wa China aliyebaki Nchini kwa ajili ya Shughuli ya Serikali ya China ambapo wamemtazama na kupitia Ripoti ambapo wameahidi kulifanyia kazi suala hilo.

Katika Mazungumzo hayo pia wamejadili Masuala mbalimbali ikiwemo Kuimarisha Usalama, Kampeni ya Ujenzi wa Ofisi za Walimu na kuongeza huduma kwa Wananchi.

RC MAKONDA pia ameishukuru Serikali ya China kwa kuleta Meli ya Jeshi la China yenye Hospital ndani ambayo imesaidia kutoa vipimo na Matibabu kwa wananchi wengi.

Kwa Upande wake Boloji Mpya wa China Nchini Tanzania WANG KE amesema Serikali ya China itaendelea kusaidiana na Tanzania katika masuala yote ya maendeleo.

Imetolewa na:-

Kitengo cha Habari na Uhusiano

**OFISI YA MKUU WA MKOA**

**DAR ES SALAAM**

30/11/2017